

MATUMIZI MABAYA YA RASILIMALI ZA TEHAMA NA MITANDAO YA MAWASILIANO YA SERIKALI

Serikali imewekeza katika kutumia TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi pamoja na utoaji huduma kwa wananchi. Katika rasilimali zinazotumika kwa wingi ni Intaneti na mtandao wa mawasiliano.

Licha ya kuwa rasilimali hizi ni kwa manufaa ya Halmashauri, kumekuwa na matumizi mabaya ya rasilimali hizo kinyume na lengo la serikali. Matumizi hayo yasiyo na tija ni pamoja na:

- matumizi ya mitandao ya kijamii wakati wa kazi
- kupakua nyaraka, picha, miziki, video pamoja na programu zenye hatimiliki bila idhini ya wamiliki.

Matumizi haya mabaya yanaleta athari kubwa katika ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi. Watu wamekua wakitumia muda mwingi wa kazi kwenye mitandao ya kijamii kuliko katika kutenda kazi.

Hivyo basi ni vyema kuhakikisha kuwa rasilimali zetu za TEHAMA zinatumika kama ilivyokusudiwa. Katika kutumia rasilimali hizo zingatia yafuatayo:

- Usipakue nyaraka, picha, video zenye hatimiliki bila idhini ya wamiliki
- Usipoteze muda wa kazi kwa kutumia mitandao ya kijamii
- Usitembelee tovuti zisizokuwa na maadili
- Usitumie rasilimali za serikali kwa matumizi binafsi yasiyikuwa na tija
- Usisambaze nyaraka za siri za serikali mtandaoni
- Tumia barua pepe rasmi za Halmashauri kwa mawasiliano ya kiofisi
- Toa taarifa ya uharibifu au matumizi mabaya ya TEHAMA
- Usitoe vifaa vya TEHAMA vya Halmashauri nje ya ofisi bila idhini

Atakae kiuka matumizi sahihi atachukuliwa hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria na miongozo.